**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU -TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI INCHUGU**
**S L.P 207,**
**TARIME.**

## MAWASILIANO:

**Mkuu wa shule 0768211920/0692386561.**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0787129898.**

**Matron Na: 0747309412.**

**Ndugu Mzazi/Mlezi wmwanafunzi**…………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI INCHUGU HALMASHAURI YA WILAYA TARIME, MKOA WA MARA MWAKA ………….**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Tano katika shule hii na atasoma tahasusi (combination)…………..

Shule hii ipo umbali wa Km saba (7) kusini mwa mji wa Sirari katika kijiji Cha Kitagasembe . Usafiri wa bodaboda toka Sirari mpaka shuleni ni 2,000/=.
Muhula wa masomo utaanza ………….. kwa hiyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni siku za kazi kuanzia tarehe …………….na mwisho wa kuripoti ni tarehe ………….na muda wa kupokelewa ni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa10:00 jioni

1. **Mambo ya kuzingatia**:-

**1.1 Sare ya shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi ndefu mbili (2) za rangi ya bluu bahari na kijani (dark green) Kitambaa kizito zenye marinda ya rinda box zinazofika kwenye kisigino.
ii. Mashati mawili (2) meupe mikono mirefu. Kwa waislamu kijuba cha rangi nyeupe na nusu kanzu isiyobana nyeupe.

iii. Viatu vya shule vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi (**visiwe vya Buti)**
iv. Sare ya michezo ni track suit rangi ya blue bahari.
v. Soksi jozi mbili nyeupe zisizo na alama yoyote
vi. Sweta ya rangi ya kijani yenye alama ya **V** shingoni.
vii. Nguo za kushindia (shamba dress) ni gauni mbili (2) za rangi ya Dark blue (kitambaa kizito) Mshono wake ni solo ndefu inayofika kwenye kisigino, yenye mikono mifupi na shingo yenye **V** kifuani. Kwa waislamu inakuwa ya mikono mirefu na kijuba kifanane na Rangi ya Shamba Dress.
viii. Huruhusiwi kusuka unatakiwa kuwa na nywele fupi.
ix. Mapambo ya aina yoyote hayaruhusiwi (mfano: kupaka rangi, kuvaa, hereni, bangiri nk.)
x. T-shirt mbili za rangi ya blue bahari na dark blue zenye kola shingoni na nembo ya shule. Pia zinapatikana shuleni kwa mzazi ambaye hatazipata kwa urahisi kwa bei ya Tshs. 15,000/=
xi. Tai mbili za rangi ya blue bahari na kijani yenye mistari myeupe. Pia zinapatikana shuleni kwa mzazi ambaye hatazipata kiurahisi kwa Tshs.5,000/= tai ya kijani na mistari myeupe na Tshs. 2,000/= kwa tai ya blue bahari.
xii. Nguo za nyumbani, manukato (perfumes),vinywaji na vyakula vya aina yoyote haviruhusiwi kabisa.

**2:1 Michango ya shule**

| Na | Aina ya mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000 |
| 2 | Tahadhari | 5,000 |
| 3 | Nembo | 5,000 |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000 |
| | Jumla Tshs | 80,000 |

**Nb:*Fedha zote zitalipwa kwenye akaunti NO 30401200169 NMB, Jina la akaunti ni Inchugu Secondari School andika jina la mwanafunzi kwenye Pay in Slip***

2:2 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

i. Ream ya karatasi moja (**A4 BOUBLE A**) kwa muhula au mbili kwa mwaka.
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi **(Orodha imeambatanishwa)**
iii. Sanduku la bati kwa ajili ya kutunzia vitu vyake.
iv. Tochi kwa tahadhari usiku umeme ukikatika
v. Madaftari makubwa (Counter books Q4) yasiyopungua saba na madaftari madogo saizi ya kati saba kwa ajili ya mazoezi.
vi. Kalamu, Rula na ufuto
vii. Scientific calculator na Mathematical Set kwa watakaosoma somo la Jiografia
viii. Godoro la Sponge la futi tatu kwa 6 na mto .
ix. Mashuka mawili rangi ya pinki, Foronya1, na chandarua cha rangi nyeupe cha mviringo.
x. Kamusi (Watakaosoma somo la Kiswahili) na English dictionary kwa wote
xi. Vyombo vya chakula (Sahani, Bakuli, Kijiko, Kikombe na Kidumu cha kutunzia maji ya kunywa)
xii. Ndoo ndogo moja na kubwa moja na kikombe kikubwa cha kuogea.
xiii. Nguo za ndani za kutosha zisizo pungua sita,aje na vesti nyeupe (spider)
xiv. Mwanafunzi aje na bima ya afya ya NHIF na kama hana awe na fedha 50,400/= ili imuwezeshe kupata Bima Bima ya afya ya NHIF

**VIFAA VYA USAFI**:

**HGL -** Jembe lenye mpini, Hard broom,Fyekeo na Dawa ya chooni lita (5) aina ya Dexi

**HKL -** Soft broom, Jembe lenye mpini na Fyekeo Dawa ya chooni Lita 5 aina ya Dexi

**SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995.Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI.Unatakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu na utapewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni;-

**3.1 Sheria na kanuni za shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulinganana ratiba ya shule.

iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation)

iv. Kuwahi katika shughuli za shule utakazopewa

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.

vii.Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kuvaa sare ya shule wakati wa vipindi na shamba dress baada ya vipindi.

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

ix. Kutunza mali zashule.

x. Ni marufuku kwa mwanafunzi kumiliki vifaa vya ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.

x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

i. **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na haruhusiwi kumpa mtumishi yeyote simu amtunzie.**

ii. **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala katika bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa**

iii. **Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda ki**

iv. **moja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hukupangiwa**

v. **Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.**

vi. **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa mkuu wa shule. (Msiba au Ugonjwa)**

v. **Kwakuwa mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni, mzazi unatakiwa kutumia simu zenye namba zilizoorodheshwa hapo juu kwa mawasiliano pamoja na kutuma fedha kwa ajili ya mwanao. Unapo tuma pesa tuma na ujumbe mfupi ukitaja jina la mwanafunzi na kiasi ulichotuma.**

**MAKOSAYATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo
iv. Kutoa lugha chafukwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yoyote yule
vi. Kusuka/Kufuga nywele ndefu au kunyoa mtindo usiokubalika
vii. Ulevi au unywaji wapombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati,uhusiano wa jinsia moja au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni uwapo shuleni
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
xiv. Kudharau Bendera yaTaifa
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

**Viambatanisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (MedicalExaminationForm) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa kituo cha afya/hospitali ya Serikali
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipaada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

iv. Picha nne(4) za Wazazi na Ndugu wakaribu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu (Picha zibandikwe kwenye Jedwali husika


v. Pia mwanafunzi ajapo shuleni muhimu awe na vitu vifuatavyo;

Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA INCHUGU SEKONDARI**

**Mkuu wa Shule**

**MURUGA P. CHACHA.**




**NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia a mitandao).Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

***TAFADHALI***

**UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE NI VYEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KWA NAMBA ZILIZOWEKWA KATIKA FOMU HII.**



**FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI PAMOJA NA AHADI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE**

Jina kamili (Kama ilivyo kwenye SelForm) ………………………….....................................

Anwani ya nyumbani………………………………………………………….. ......

Tarehe ya kuzaliwa …………………........................................

Mahali ulipozaliwa, Kijiji…………………………..Kata…………………………...Tarafa………………

Wilaya…………………………. Mkoa………………………………..

Mahali unapoishi kwa sasa………………………………………….

Shule ya Sekondari ulikotoka … .......................................................................

Anwani ya shule ……………………………….....................................................

Dini/Dhehebu………………………………………………………………..

Kabila………………………………………………………………………….

Baba na Mama wanaishi au hawaishi?(a) Baba……………….. (b)Mama …………………

Jamaa katika familia ambao wanaweza kupelekewa taarifa zako muhimu

| SN | JINA | PICHA | UHUSIANO | KAZI | NAMBAYA SIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | |
| 2 | | | | | |
| 3 | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| 4 | | | | | |

## KWA MASUALA YA SHULE

**Ahadi yautii:**

Mimi (Mwanafunzi)………………………………………nathibitisha kuwa taarifa nilizozijaza hapo juu ni za kweli.Ahadi yangu, nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa naTaifa kujiunga na shule hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule hii kama zilivyotolewa na zitakavyotole

………………………………… ………………………….

Sahihi ya Mwanafunzi Tarehe

Mimi(Jina la Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi)…………………………………………………… ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi ……………………………………………………. nimeyasoma masharti na sheria za **SHULE YA SEKONDARI INCHUGU** ambako binti yangu amechaguliwa kujiunga.Naahidi kwamba nitamuhimiza mwanangu kufuata sheria na taratibu zote za shule kama zilivyoelezwa na kumtimizia mahitaji yake na kulipa ada ya shule na michango mingine yote. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora na mwema wa Taifa letu.

…………………… …………………

SahihiyaMzazi/Mlezi Tarehe

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**INCHUGU SECONDARY SCHOOL,**
**P.O.Box 207,**
**TARIME.**

**To Medical Officer,**
**...........................................................**
**Ref…………………………………….....................(NAME OF STUDENT)**

Please examine the above named Student as per Medical examination form below,

(To becompleted by Government Medical Officer)

Full Name………………………………Age…………Height………… (cm) Weight .............. (Kg)
Bloodcount (Red and White)…………………………………………………………………..
Stool Examination…………………………………………………………………………………
Urinary analysis…………………………………………………………………………………..
STDs and other V.D………………………………………………………………………………
T.B……………………………………………………………………………………………………..
Leprosy test ……………………………………………………………………………..........
Eye test…………………………………………………………………………………………
Ear test…………………………………………………………………………………………….
Chest…………………………………………………………………………………………………
Abdominal test…………………………………………………………………………………..
Blood Group **(Very Crucial)**………………………………………………………………………
Spleen………………………………………………………………………………………………
Pregnancy test…………………………………………………………………………………..
Bilharzias……………………………………………………………………………………………..
Asthma………………………………………………………………………………………………
Skin diseases……………………………………………………………………………………….
Any additional defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g.Sicklecell)
……………………………………………………………………………………………………………………………

***I have examined the above named student and I certify that she is FIT/NOT FIT to pursue Secondary Education.***

***Signature……………………………………….Date…………………………..***

***Station……………………………………………………………………………***

**Designation and Official Stamp ……………………………………………………..**

**ORODHA YA VITABU VYA MASOMO YA TAHASUSI MWANAFUNZI ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO**

**KISWAHILI:**

Kito cha lugha Kidato cha Tano na Sita- Lubandaja ( Mtaala Mpya 2023)
Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha 5 & 6.
Nyambari Nyangwine (Mtaala Mpya 2023)
Kiswahili Fasaha kidato cha 5 & 6 Oxford ( Mtaala Mpya 2023)

**TAHAKIKI ZA VITABU**

**Riwaya.**
Dunia uwanja wa fujo.
Uwa la faraja.
Wasifu wa Biti Binti Saadi.
Mirathi ya hatari.

**Tamthiliya.**
Mkwawa wa Uhehe.
Shujaa Mirambo.
Usaliti Mjini.
Nyerere na safari ya Kanani.

**Ushairi**
Dhifa
Utenzi Majumui wa karne ya 21.
Malenga wa Bara
Fungate ya Uhuru
Fumbo linaloelea
Malenga wa ziwa kuu
Andamo Msafiri safarini
Wosia wa

**ENGLISH:**

**Novel.**
Animal farm
Chasing the leopard finding the lion
The Oppotunist elite, The horizon unveiled,

**Play.**
The government Insepector, The enemy of the people,A taste of heaven,

**Poetry**.
Surmons, Poets of Africa